# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani, Buyu,
70490 Mjini Magharibi,
S.L.P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 2242000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA BAJETI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO (WFM) KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia afya njema, uhai na uwezo wa kukutana tena katika Baraza hili Tukufu kwa madhumuni ya kuendelea kuwawakilisha wananchi wa Zanzibar kwa kutekeleza majukumu mbalimbali tuliyokabidhiwa kwa niaba yao. Leo hii tumekutana hapa kwa ajili ya kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango (WFM) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya kipekee, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Baraza kwa uongozi wenu wenye hekima, weledi na usimamizi mzuri wa shughuli za Baraza hili Tukufu. Uongozi wenu umeendelea kutuwezesha Wajumbe wa Baraza kutekeleza majukumu yetu kwa utulivu, nidhamu na ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda pia kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati pamoja na pongezi maalum kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake madhubuti, wenye maono na wenye kuendelea kuiletea nchi yetu maendeleo katika nyanja mbalimbali. Tunatambua juhudi kubwa anazoendelea kuzichukua katika kuimarisha uchumi, huduma za kijamii na ustawi wa wananchi, sambamba na dhamira yake ya dhati ya kutekeleza ahadi alizozitoa kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hayo, napenda kutoa shukrani na pongezi za pekee kwa Makamo wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, kwa kuendelea kutoa ushirikiano wa karibu kwa Mheshimiwa Rais katika kusimamia shughuli za

Serikali na kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Kwa hakika, kwa pamoja wameendelea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, busara na uzalendo mkubwa, hali inayochangia kuimarika kwa utendaji wa Serikali na utekelezaji wa sera na mipango ya maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kutoa shukrani za dhati kwa Waziri wa Fedha na Mipango (WFM) Mhe. Dkt. Juma Malik Akil, Naibu Waziri, Mhe. Dkt. Hamad Omar Bakar pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango (WFM) wakiongozwa na Kaimu Katibu Mkuu, CPA Aboud Hassan Mwinyi, kwa ushirikiano wao wa karibu na wa dhati walioutoa kwa Kamati ya Bajeti. Ushirikiano huo umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na weledi mkubwa. Ni matumaini yangu kuwa, mashirikiano haya yataendelea kuimarika siku hadi siku, na hivyo kuongeza ufanisi zaidi katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati ya Bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Kadhalika, napenda kuwapongeza kwa dhati watendaji wa Idara ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango (WFM) wakiongozwa na Ndugu Zena Mahmoud Hassan, pamoja na Maafisa Mipango na watendaji wote wa Wizara na taasisi zote za Serikali waliohusika katika zoezi la kuingiza taarifa za bajeti katika Mfumo wa Bajeti na Matumizi Serikalini. Kwa hakika, wameonesha juhudi kubwa, umahiri na kujituma kwa hali ya juu katika kutekeleza jukumu hilo muhimu. Kamati ya Bajeti inatambua na kuthamini mchango wao mkubwa katika kufanikisha zoezi hilo. Tunawasisitiza waendelee kudumisha ari, moyo wa kujituma na uzalendo huo huo katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku kwa manufaa ya nchi yetu na wananchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa matakwa ya Kanuni ya 101(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2024, ambayo inaelekeza Kamati kupitia na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kabla ya kuwasilishwa na kujadiliwa katika Baraza lako Tukufu. Kamati ya Bajeti ilitekeleza wajibu wake huo kwa kupitia na kufanya uchambuzi wa kina wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango (WFM) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** Kukamilika kwa Hotuba hii kumetokana na michango na mashirikiano ya Wajumbe wa Kamati ya Bajeti. Kwa msingi huo, napenda kuwapongeza kwa dhati kwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi mkubwa. Vilevile, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti kwa kuratibu kwa ufanisi shughuli zote za Kamati pamoja na kuendelea kutoa ushauri wa

kitaalamu unaosaidia kwa kiasi kikubwa kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Kwa ruhusa yako Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue kwa majina Wajumbe pamoja na Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ali Suleiman Ameir | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Maryam Said Khamis | Makamo Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Bakar Hamad Bakar | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Farida Amour Mohammed | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mohammed Ali Salim | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Sulubu Kidongo Amour | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Yussuf Ali Hassan | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |
| 9. | Ndg. Maryam Mohammed Othman | Katibu |
| 10. | Ndg. Shaib Fadhil Shaib | Katibu |
| 11. | Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi | Katibu |
| 12. | Ndg. Said Bakar Hamad | Msaidizi wa Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi na shukran hizo, sasa naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango (WFM) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Maoni haya yamejikita katika uchambuzi wa Kamati katika mafungu saba (7) yanayosimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango (WFM), Fungu F01 - Wizara ya Fedha na Mipango, Fungu F02 - Mfuko Mkuu wa Serikali, Fungu F03 - Tume ya Mipango, Fungu F04 - Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Fungu F05 - Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Fungu F06 - Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali, na Fungu F07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO (WFM) KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu zinaonesha kwamba, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Fedha na Mipango (WFM) ilikadiriwa kukusanya jumla ya TZS 6,527.599 bilioni kupitia mafungu yake ya F01, F04, F05 na F07. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, lengo la ukusanyaji lilikuwa TZS 4,351.313 bilioni, ambapo hadi kufikia Machi 2026 jumla ya TZS 3,217.341 bilioni zilikuwa zimekusanywa, sawa na asilimia 74 ya lengo la makusanyo kwa kipindi hicho. Kamati inaipongeza Wizara ya Fedha na Mipango kwa mafanikio yaliyopatikana katika ukusanyaji wa mapato hayo. Hata hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuendelea kuimarisha usimamizi wa vyanzo vya mapato, kuziba mianya ya upotevu wa mapato na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji ili kufikia

kikamilifu malengo yaliyowekwa

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Fedha na Mipango (WFM) ilikadiriwa kutumia jumla ya TZS 1,571.151 bilioni kupitia mafungu yake ya F01, F02, F03, F04, F05, F06, na F07. Kwa kipindi cha Julai – Machi 2026, Wizara imepangiwa kutumia TZS 1,280.912 bilioni ambapo hadi kufikia Machi 2026 TZS 1,154.017 bilioni zimetumika, sawa na asilimia 90 ya makadirio ya katika kipindi cha tathmini. Kamati inaishauri Wizara kuendelea kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha ili kuhakikisha utekelezaji wa shughuli na programu zilizopangwa unafanyika kwa ufanisi na kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa.

**Mheshimiwa Spika,** Mchanganuo wa mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mujibu wa mafungu ni kama ifuatavyo:

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuanzia na mapato ya Fungu F01 - Wizara ya Fedha na Mipango, katika mwaka wa fedha 2025/2026 lilikadiriwa kukusanya TZS 3,518.629 bilioni. Aidha, katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, Fungu hilo lilitarajia kukusanya TZS 2,085.511 bilioni na kufanikiwa kukusanya TZS 2,013.861 bilioni, sawa na asilimia 97 ya makadirio ya kipindi hicho. Kwa upande wa matumizi, Fungu F01 limepangiwa kutumia TZS 866.134 bilioni katika mwaka wa fedha 2025/2026 ambapo hadi kufikia Machi 2026, limetumia TZS 549.679 bilioni sawa na asilimia 88 ya makadirio ya TZS 622.475 bilioni ya kipindi cha tathmini. Miongoni mwa matumizi yaliyofanyika ni kupitia Programu Kuu ya Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma, ambayo imepangiwa kutumia TZS 138.345 bilioni kwa mwaka, na hadi Machi 2026 ilikuwa imetumia TZS 27.257 bilioni sawa na asilimia 66 ya makadirio ya TZS 41.230 bilioni ya kipindi cha tathmini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Wizara kwa kufikia kiwango kikubwa cha makusanyo ya mapato. Hata hivyo, inaishauri kuondoa changamoto zilizopo katika mfumo wa Zan Malipo ili kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato, pamoja na kuharakisha zoezi la kuhamishia mapato yote yasiyo ya kodi kukusanywa na ZRA. Aidha, kutokana na umuhimu wa Programu ya Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma katika kusimamia mapato, matumizi na bajeti inayozingatia jinsia na usawa, Kamati inaishauri Wizara kueleza bayana hatua zilizofikiwa na Wizara nane za majaribio zinazotekeleza mpango huo.

**Mheshimiwa Spika,** Fungu la Pili linalosimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango ni Fungu F02 – Mfuko Mkuu wa Serikali, ambalo kwa mwaka wa fedha 2025/2026

limepangiwa kutumia TZS 641.350 bilioni. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026, Fungu hilo limetumia TZS 561.07 bilioni sawa na asilimia 92 ya makadirio ya TZS 608.725 bilioni, ambapo matumizi haya yamehusisha pensheni kwa wazee na wastaafu pamoja na matumizi mengine muhimu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kamati inaipongeza Wizara kwa usimamizi mzuri wa fungu hili katika kuhakikisha kunaendelea kuwepo nidhamu ya matumizi ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Fungu la tatu ni Fungu F03 – Tume ya Mipango Zanzibar ambalo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 limepangiwa kutumia TZS 20.380 bilioni. Katika kipindi cha Julai - Machi 2026, Tume ilitumia TZS 16.513 bilioni sawa na asilimia 93 ya makadirio ya TZS 17.848 bilioni ya kipindi cha tathmini. Kupitia Programu Kuu ya Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendaji, ambayo inalenga kuimarisha uratibu wa mipango ya maendeleo ya kitaifa pamoja na ufuatiliaji na tathmini, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, programu hii limepangiwa kutumia jumla ya TZS 14.786 bilioni, ambapo hadi kufikia Machi 2026 limetumia TZS 13.993 bilioni sawa na asilimia 106 ya makadirio ya TZS 13.258 bilioni ya kipindi cha tathmini. Kutokana na umuhimu wa eneo hili katika uandaaji na usimamizi wa mipango ya maendeleo ya nchi, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha upatikanaji wa Mpango mpya wa Maendeleo wa Zanzibar, ikizingatiwa kuwa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) uliopo unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa Juni 2026.

**Mheshimiwa Spika,** Fungu la nne ni Fungu F04 – Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi imekadiriwa kukusanya TZS 180 milioni, ambapo katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026 ilikadiriwa kukusanya TZS 130 milioni na hadi Machi 2026 imekusanya TZS 61 milioni sawa na asilimia 47, hali inayoonesha kuwa makusanyo bado si ya kuridhisha. Aidha, kwa upande wa matumizi, Fungu hili limepangiwa kutumia TZS 11.607 bilioni katika mwaka wa fedha 2025/2026, ambapo hadi Machi 2026 limetumia TZS 7.894 bilioni sawa na asilimia 105 ya makadirio ya TZS 7.523 bilioni ya kipindi cha tathmini.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na hali ya mwenendo mapato na matumizi katika fungu hili, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kuvitathmini vyanzo vyake vya mapato, kuweka mikakati madhubuti ya kuongeza makusanyo, sambamba na kusimamia kikamilifu taratibu za matumizi ili kuhakikisha yanazingatia mipango iliyoidhinishwa na kutoa tija iliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Fungu la tano ni Fungu F05 – Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Katika kwa mwaka wa fedha 2025/2026, fungu hili limekadiriwa kukusanya TZS 2,980.289 bilioni, ambapo katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026 limefanikiwa kukusanya TZS 1,187.315 bilioni sawa na asilimia 53 ya makadirio ya TZS 2,240.411 bilioni ya kipindi hicho. Hali hii inayoonesha upungufu wa makusanyo unaohitaji kuimarishwa. Kwa upande wa matumizi, Fungu hili limepangiwa kutumia TZS 17.589 bilioni katika mwaka wa fedha 2025/2026, ambapo hadi kufikia Machi 2026 fungu hili limetumia TZS 10.532 bilioni sawa na asilimia 78 ya makadirio ya TZS 13.444 bilioni. Katika fungu hili Programu Kuu ya Usimamizi wa Hazina inayohusika na usimamizi wa fedha za umma, usuluhishi wa hesabu za mapato, Deni la Taifa na Mfuko Mkuu, ambapo imepangiwa kutumia TZS 2.729 bilioni na imetumia TZS 880 milioni sawa na asilimia 39 ya makadirio ya TZS 2.266 bilioni ya kipindi cha tathmini.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na mwenendo huu wa mapato na matumizi, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuongeza usimamizi wa makusanyo ili kufikia malengo na kuziba mianya ya upotevu wa mapato, kusimamia ipasavyo mapato yatokanayo na uendeshaji wa masoko ili kurejesha fedha za ujenzi katika Mfuko Mkuu wa Serikali, kuweka mikakati ya kuhakikisha kasi ya ongezeko la Deni la Taifa inaendana na ulipaji wake, pamoja na kufanya uhakiki wa kitaalamu wa mfumo wa Bajeti na Matumizi ya Serikalini (BAMAS) ili kubaini na kutatua changamoto zinazoukabili mfumo katika uingizaji wa taarifa za bajeti za Wizara na taasisi za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Fungu la Sita ni Fungu F06 – Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali ambapo kupitia Programu Kuu ya Usimamizi wa Ukaguzi wa Ndani Serikalini, hadi kufikia Machi 2026 programu hii imetumia TZS 256 milioni sawa na asilimia 26 ya makadirio ya TZS 991 milioni ya kipindi cha tathmini. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi imepangiwa kutumia TZS 6.479 bilioni, ambapo katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026 imetumia TZS 3.808 bilioni sawa na asilimia 76 ya makadirio ya TZS 5.038 bilioni ya kipindi hicho.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kuweka bayana mambo muhimu yaliyobainika katika kaguzi zilizofanyika katika taasisi za Serikali, sambamba na Ofisi kuwa na ufanisi zaidi katika kutumia miongozo ya ukaguzi kwa taasisi za Serikali na kuandaa ripoti zitakazotoa matokeo ya ukaguzi pamoja na hatua zinazohitajika kuchukuliwa ili kuimarisha uwajibikaji, uwazi na utawala bora.

**Mheshimiwa Spika,** Fungu la Saba ni Fungu F07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina, ambayo

ina jukumu la kusimamia mali za umma na uwekezaji katika mashirika ya umma. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi hii imekadiriwa kukusanya TZS 28.5 bilioni, ambapo katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026 ilipangiwa kukusanya TZS 25.26 bilioni na kufanikiwa kukusanya TZS 16.104 bilioni sawa na asilimia 64 ya makadirio yaliyopangwa. Kwa upande wa matumizi, katika kutekeleza majukumu yake, Ofisi ilipangiwa kutumia TZS 7.609 bilioni, ambapo hadi Machi 2026 imekadiriwa kutumia TZS 5.856 bilioni na imetumia TZS 4.52 bilioni sawa na asilimia 77 ya makadirio. Kupitia Programu Kuu ya Usimamizi wa Mali za Umma na Uwekezaji pamoja na Programu ya Uendeshaji na Utawala, Ofisi imeweza kuandaa miongozo mitano itakayosaidia kuimarisha na kurahisisha usimamizi wa mashirika ya umma yenye mchango mkubwa katika gawio kwa Serikali na utoaji wa huduma.

**Mheshimiwa Spika,** Fungu hili linahusika pia na ukusanyaji wa mapato yatokanayo na ukodishaji wa mashamba. Awali, mapato haya yalikuwa yakikusanywa na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, kwa kuzingatia kuwa usimamizi wa mashamba hayo pamoja na gharama zote zinazohusiana na ukuzaji na matunzo ya mazao yaliyomo ndani yake unasimamiwa na Wizara hiyo mapato hayo yanakusanywa kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina. Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kufikia makubaliano kuhusu usimamizi wa mapato yatokanayo na ukodishaji wa mashamba.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO INAYOSIMAMIWA NA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO (WFM) KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Fedha na Mipango (WFM) ilipanga kutekeleza programu tano (5) pamoja na miradi saba (7) ya maendeleo, ambapo hadi kufikia Machi 2026 imefanikiwa kutumia TZS 517.981 bilioni sawa na asilimia 73 ya makadirio ya TZS 707.017 bilioni kwa mwaka mzima wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Fedha na Mipango katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 imetekeleza Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali ambapo jumla ya TZS 126.298 bilioni zimekadiriwa na matumizi yaliyofanyika ni TZS 67.992 bilioni sawa na asilimia 54. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa Taasisi ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi, Shirika la Magazeti Tunguu, Ofisi ya Nyaraka Kilimani, Chuo cha Utawala wa Umma Pujini Pemba, pamoja na kuanza ujenzi

wa Mji wa Serikali na Baraza la Wawakilishi Kisakasaka. Kamati inaishauri Wizara kuendelea na utekelezaji wa programu hii katika bajeti ya 2026/2027 kwa kuzingatia gharama na muda uliopangwa, sambamba na kuimarisha usimamizi ili kuhakikisha majengo yanakamilika kwa ubora unaostahili na kuwezesha watumishi kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Miradi mengine inayotekelezwa ni Mpango Kabambe wa Uimarishaji wa Takwimu Tanzania Awamu ya Pili pamoja na Mradi wa Uimarishaji wa Takwimu za Jinsia ambayo kwa pamoja inalenga kuimarisha mfumo wa takwimu Zanzibar ili kuwezesha upatikanaji na matumizi ya takwimu kwa wakati, pamoja na kuhakikisha takwimu za jinsia zinasaidia katika uandaaji wa sera na mipango inayozingatia mahitaji ya makundi yote. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, miradi hii imetumia jumla ya TZS 4.885 bilioni, ambapo Mpango Kabambe umetumia TZS 4.086 bilioni sawa na asilimia 89 ya makadirio ya TZS 4.598 bilioni, na Mradi wa Takwimu za Jinsia umetumia TZS 799 milioni sawa na asilimia 34 ya makadirio ya TZS 2.32 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli zilizotekelezwa katika miradi hii ni pamoja na kukamilisha ukusanyaji wa taarifa za utafiti wa mapato na matumizi ya kaya, utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi kwa mwaka 2024/2025, pamoja na kutoa mafunzo ya uratibu wa takwimu za jinsia kwa taasisi za Serikali. Kamati inaipongeza Wizara kwa utekelezaji wa miradi hii kwani itaimarisha uchambuzi wa takwimu na kusaidia kufanya maamuzi sahihi ya mipango ya maendeleo. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuongeza usimamizi katika eneo la upatikanaji wa fedha za Mradi wa Takwimu za Jinsia ili kuondoa changamoto ya utekelezaji mdogo uliobainika, sambamba na kuimarisha uwezo wa taasisi husika katika ukusanyaji, uchambuzi na matumizi ya takwimu ili ziweze kutumika ipasavyo katika kupanga na kutekeleza sera na mipango ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa miradi mengine ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Fedha na Mipango, Kamati imebaini kuwa miradi hiyo imeendelea kutekelezwa kwa mafanikio katika maeneo mbalimbali ya kiuchumi, kijamii na kiutawala, ikiwa ni sehemu ya juhudi za Serikali katika kuimarisha utendaji wa taasisi na utoaji wa huduma kwa wananchi. Miradi hiyo ni pamoja na Programu ya Ukuzaji wa Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z) ambayo imeendelea kuimarisha miundombinu ya utalii, usimamizi wa taka na kujenga uwezo wa maafisa katika masuala ya kodi na fedha; Programu ya Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP-VI) ambayo

imeimarisha mapitio ya sera na sheria, utafiti wa mifumo ya fedha na kujenga uwezo wa watumishi; pamoja na Mradi wa Uimarishaji Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili (ISP-DRM) unaolenga kuimarisha mapato ya ndani na kusimamia sekta ya mafuta, gesi na madini kupitia uandaaji wa sera na sheria husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine, Kamati imebaini kuwa Programu ya Urasimishaji Ardhi na Biashara Zanzibar imeendelea kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia utoaji wa hati za ardhi, uimarishaji wa masjala na matumizi ya mifumo ya kidigitali pamoja na mafunzo kwa watendaji; Mradi wa Uratibu na Usimamizi wa Mipango ya Maendeleo umeendelea kuimarisha uratibu wa miradi, uthamini wa fidia, uandaaji wa miongozo na uanzishaji wa mfumo jumuishi wa mipango ya maendeleo; na Mradi wa Mapitio, Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini ya Mipango ya Maendeleo umeimarisha ufuatiliaji wa miradi, uandaaji wa ripoti za SDGs, tathmini ya ZADEP na kujenga uwezo wa watendaji wa ufuatiliaji na tathmini.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi mwengine ni Mradi wa Kuendeleza Tafiti za Kimkakati Zanzibar ambao umeendelea kuimarisha tafiti na ubunifu kwa kuandaa miongozo ya utafiti, kufanya tathmini ya ajenda za utafiti na kuandaa mikakati ya maendeleo ya mazao ya kimkakati kama karafuu na chumvi; na Mradi wa Utekelezaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu (IPSAS Accrual) umeendelea kuimarisha uwazi wa taarifa za fedha kupitia mafunzo, uandaaji wa miongozo, kuimarisha wa mifumo ya uhasibu na ushirikiano wa kitaalamu katika uandaaji wa hesabu za Serikali.

## TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAPATO NA MATUMIZI YA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO (WFM) KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** Tathmini ya Utekelezaji wa Mapato na Matumizi ya Taasisi zinazosimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango (WFM) kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 imeonesha kwa ujumla mafanikio ya baadhi ya taasisi hizo kufikia na hata kuvuka malengo ya makusanyo, sambamba na kuwepo kwa changamoto katika taasisi chache ambazo hazijafikia viwango vilivyotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) imekusanya TZS 826.974 bilioni sawa na asilimia 94 ya lengo la TZS 878.579 bilioni katika kipindi cha Julai 2025

hadi Machi 2026, na kwa upande wa matumizi imetumia TZS 23.480 bilioni sawa na asilimia 97 ya makadirio ya TZS 24.04. Kamati inaipongeza Mamlaka kwa mafanikio hayo, hata hivyo, Kamati inaishauri ZRA kuendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwa kupanua wigo wa walipa kodi, hususan kwa kuwabaini na kuwasajili wafanyabiashara wa mtandaoni wanaofanya shughuli zao nje ya Zanzibar lakini wakihudumia soko la Zanzibar. Vilevile, ZRA inapaswa kuimarisha utambuzi na ufuatiliaji wa kampuni za kigeni zinazoleta watalii Zanzibar, hususan kwa kufuatilia malipo yanayofanywa na watalii nje ya Zanzibar kabla ya kuwasili nchini. Hatua hizi zitasaidia kuongeza uwazi katika miamala ya sekta ya utalii, kupunguza upotevu wa mapato na hatimae kuongeza mchango wa sekta hiyo katika mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa upande wa Zanzibar imekusanya TZS 616.505 bilioni sawa na asilimia 102 ya lengo la TZS 605.773 katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026. Kamati inaipongeza TRA kwa kufikia malengo hayo, hata hivyo Kamati inaisisitiza kuimarishwa mawasiliano baina ya TRA, Wizara ya Ardhi na taasisi nyengine za Serikali ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na uuzaji wa rasilimali kama vile ardhi na majengo, ambapo chanzo hicho bado hakijafikia malengo yaliyotarajiwa, licha ya kuwepo kwa shughuli kubwa za biashara za uuzaji wa viwanja na hoteli zinazofanyika kwa kiasi kikubwa katika maeneo mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) imekusanya TZS 201 bilioni sawa na asilimia 90 ya lengo la TZS 223 bilioni katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026. Ili kuongeza ufanisi na utoaji wa huduma bora, Kamati inaishauri Serikali kuiongezea mtaji katika benki ya PBZ ambayo inamilikiwa kwa asilimia 100, ili kuwa na uwezo wa kupanua huduma zake nchini, pamoja na kuimarisha mafunzo kwa watumishi ili kuongeza weledi, ufanisi na ushindani katika sekta ya kibenki.

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma Zanzibar (ZPPRA) imekusanya TZS 410 milioni sawa na asilimia 48 ya makadirio ya TZS 857 milioni kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2026. Kwa lengo la kuimarisha makusanyo ya Mamlaka kupitia ada za nyaraka za zabuni, ada ya mafunzo ya ununuzi na vyanzo vyengine mbalimbali, Kamati inaishauri kuhakikisha kuwa inaimarisha ukusanyaji wa mapato ili yaendane na hali halisi ya shughuli za manunuzi ambazo zinafanyika kwa kiwango kikubwa. Aidha Kamati inaitaka Mamlaka kuendelea kutoa mafunzo ya sheria mpya ya manunuzi pamoja na Kanuni zake kwa Maafisa Manunuzi wa Serikali na wadau

mbalimbali kwa lengo la kuimarisha shughuli za manunuzi ya Serikali ambayo yataleta tija na kupunguza mianya ya ubadhirifu wa fedha umma.

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) limekusanya TZS 122.9 bilioni sawa na asilimia 112 ya lengo la TZS 109.7 bilioni katika kipindi cha Julai hadi Machi 2026. Kamati inalipongeza Shirika kwa kuvuka malengo ya ukusanyaji wa mapato, hata hivyo, kwa lengo la kuongeza mapato na kuweka ulinzi katika miradi ya maendeleo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha miradi ya maendeleo bima.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) umepangiwa kukusanya mapato ya TZS 281.33 bilioni ambapo makusanyo halisi ni TZS 346.35 bilioni sawa na asilimia 123. Kamati inaipongeza ZSSF kwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato hali inayowezesha ZSSF kulipa mafao kwa wanachama na kuendeleza shughuli za uwekezaji. Aidha, Kamati inaishauri ZSSF kuendelea kuimarisha mifumo yake ya TEHAMA katika utoaji wa huduma kwa wanachama wake ili kurahisisha shughuli za usajili pamoja na kuweka kumbukumbu za kidigitali kwa lengo la kurahisisha utoaji wa mafao kwa wakati na kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar (ZIAAT) kwa kipindi cha Julai – Machi 2026 imekusanya jumla ya TZS 201 milioni ikiwa ni sawa na asilimia 61 ya makadirio ya TZS 328 milioni. Kamati inaishauri taasisi hii kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuendelea kutoa mafunzo kwa watendaji wake pamoja na wataalamu wengine wa uhasibu na kodi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF) umefanikiwa kukusanya TZS 48.04 bilioni sawa na asilimia 78 ya lengo la kukusanya TZS 61.43 bilioni. Kamati inaushauri Mfuko kuimarisha utoaji wa huduma kwa kuendelea kusajili wanachama wapya, sambamba na kuimarisha mifumo ya udhibiti ili kupunguza mianya ya upotevu wa fedha. Vilevile, Mfuko unapaswa kusimamia kwa karibu watoa huduma wasio waaminifu wanaowasilisha madai yasiyoendana na huduma halisi zilizotolewa, ambapo mara nyingi malipo yanakuwa makubwa kuliko uhalisia wa huduma zilizotolewa katika vituo vya afya.

## TATHMINI YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO (WFM) KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Fedha na Mipango

inatarajiwa kukusanya jumla ya TZS 8,052.83 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 23 ukilinganisha na makadirio ya kukusanya TZS 6,527.59 bilioni katika mwaka wa fedha 2025/2026. Mapato haya yatakusanywa kupitia mafungu Fungu 009 – Wizara ya Fedha na Mipango, Fungu 022 – Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Fungu 023 – Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, na Fungu 106 – Ofisi ya Msajili wa Hazina. Katika makadirio hayo, Fungu 009 linatarajiwa kukusanya kiasi kikubwa cha TZS 7,772.441 bilioni, likifuatiwa na Fungu 022 litakalokusanya TZS 246.277 bilioni. Aidha, Fungu 106 linakadiriwa kukusanya TZS 34 bilioni, na Fungu 023 likichangia TZS 112 milioni. Kwa ujumla, makadirio haya yanaonesha mchango wa kila fungu katika kufanikisha malengo ya ukusanyaji wa mapato ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Fedha na Mipango (WFM) inakadiria kutumia jumla ya TZS 2,078.925 bilioni katika mafungu yake mbalimbali, ikiwa ni hatua muhimu katika kuendeleza utekelezaji wa majukumu yake. Mgawanyo wa fedha za matumizi kama ifuatavyo: Fungu 009 – Wizara ya Fedha na Mipango limekadiriwa kutumia TZS 1,322.884 bilioni, Fungu 021 – Mfuko Mkuu wa Serikali limekadiriwa kutumia TZS 576.693 bilioni, Fungu 022 – Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali limekadiriwa kutumia TZS 17.028 bilioni, Fungu 023 – Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali limekadiriwa kutumia TZS 14.004 bilioni, Fungu 024 – Tume ya Mipango limekadiriwa kutumia TZS 34.156 bilioni, Fungu 052 – Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali limekadiriwa kutumia TZS 6.875 bilioni, na Fungu 106 – Ofisi ya Msajili wa Hazina limekadiriwa kutumia TZS 107.284 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inayaafiki makadirio haya sambamba na kuishauri Serikali kuendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha za umma, hususan kwa kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA. Vilevile, Kamati inasisitiza umuhimu wa kuimarisha nidhamu ya mapato na matumizi ya fedha za umma, kwa kuhakikisha ukusanyaji wa mapato unafanyika kikamilifu kulingana na makadirio, na matumizi yanafuata mipango iliyoidhinishwa. Hatua hizi zitasaidia kuongeza uwazi na uwajibikaji, kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa bajeti, pamoja na kupunguza au kuondoa kabisa mianya ya upotevu wa fedha za umma.

## TATHMINI YA MAPENDEKEZO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO INAYOSIMAMIWA NA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO (WFM) KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Fedha na Mipango (WFM) kwa mwaka wa fedha 2026/2027 inatarajia kutekeleza miradi na programu mbalimbali za maendeleo zenye lengo la kuimarisha uchumi jumuishi, kuimarisha usimamizi wa fedha za umma na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya nchi yetu. Miradi hiyo inajumuisha Programu ya Ukuzaji wa Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z) inayolenga kuinua ustawi wa wananchi katika maeneo ya mjini kwa gharama ya TZS 32 bilioni, pamoja na Programu ya Mageuzi ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP IV) inayolenga kuimarisha uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika matumizi ya fedha za umma kwa gharama ya TZS 3.241 bilioni.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara pia itaendelea na utekelezaji wa mradi wa Ujenzi na Uimarishaji wa Ofisi za Serikali kwa gharama ya TZS 166.964 bilioni. Vilevile, imepanga kutekeleza programu za kuimarisha uchumi jumuishi kupitia urasimishaji wa biashara na ardhi, uimarishaji wa tafiti za kimkakati, pamoja na kuimarisha mifumo ya takwimu kupitia Mpango Kabambe wa Uimarishaji Takwimu Tanzania Awamu ya Pili (TSMP II) na mradi wa Uimarishaji wa Takwimu za Jinsia.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuhakikisha matokeo yaliyokusudiwa katika utekelezaji wa miradi na programu hizi yanafikiwa kwa ufanisi na tija, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa utekelezaji wa miradi na programu zote za maendeleo zilizoainishwa unazingatia mipango iliyowekwa, muda na thamani ya fedha (value for money). Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa karibu wa miradi hiyo ili kudhibiti ucheleweshaji, ongezeko la gharama zisizo za lazima na kuhakikisha uwajibikaji wa watendaji katika kila hatua ya utekelezaji.

## TATHMINI YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO (WFM) KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango (WFM) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 inaonesha taasisi zinazosimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango (WFM) kuwa katika mwelekeo chanya wa ukuaji wa mapato, uimarishaji wa huduma na kuongeza mchango katika uchumi wa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa taasisi za ukusanyaji wa mapato, Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) imepangiwa kukusanya TZS 1,726.66 bilioni, sawa na ongezeko

la asilimia 37 kutoka TZS 1,257.24 bilioni za mwaka uliopita, ambapo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Zanzibar ikitarajiwa kukusanya TZS 1,144.69 bilioni ikilinganishwa na TZS 825.769 bilioni za mwaka 2025/2026, sawa na ongezeko la asilimia 38.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaona ongezeko hili linaashiria kuendelea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi pamoja na mafanikio ya juhudi za Serikali katika kutanua wigo wa walipakodi na kudhibiti uvujaji wa mapato. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha matumizi ya teknolojia za kisasa, kupashana taarifa kati ya taasisi za Serikali ili kubaini ukwepaji wa kodi na tozo hususan katika sekta za biashara za kidijitali, utalii na uwekezaji ili kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa taasisi za kifedha na hifadhi ya jamii, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) unatarajia kukusanya TZS 541.03 bilioni kupitia michango ya wanachama na mapato ya uwekezaji, wakati Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) inatarajia kufikia mapato ya TZS 322.9 bilioni, kupata faida ya TZS 142.6 bilioni na kuongeza amana za wateja hadi TZS 2,767.5 bilioni. Vilevile, Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) linatarajia kukusanya TZS 163.7 bilioni. Kamati inazipongeza taasisi hizi kwa mwelekeo mzuri wa ukuaji wa mapato, lakini inazisisitiza kuendelea kuimarisha usimamizi wa uwekezaji, ukusanyaji wa michango na madeni, pamoja na kuongeza ubunifu katika huduma za kidijitali ili kuongeza ushindani, na kuimarisha uhimilivu wa kifedha.

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi za udhibiti na taaluma nazo zina mchango muhimu katika kuimarisha usimamizi wa fedha za umma. Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma Zanzibar (ZPPRA) inatarajia kukusanya TZS 910 milioni pamoja na kupokea ruzuku ya TZS 3.488 bilioni, huku Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar (ZIAAT) ikitarajia kukusanya TZS 667 milioni na kupokea ruzuku ya TZS 3.042 bilioni. Kamati inaishauri taasisi hizi kuendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi wa mapato, matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma, pamoja na kuimarisha mifumo ya uwajibikaji na udhibiti wa taarifa za kifedha ili kuongeza ufanisi wa utendaji wao.

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF) unatarajia kukusanya TZS 124.42 bilioni katika mwaka wa fedha 2026/2027, ambapo fedha hizo zitatumika kugharamia shughuli za uendeshaji, miradi ya maendeleo na uwekezaji kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi. Kamati inaupongeza Mfuko kwa

mwelekeo huo na kuushauri kuendelea kuimarisha mifumo ya malipo kwa watoa huduma za afya ikiwemo hospitali na vituo vya afya ili kuhakikisha malipo yanafanyika kwa wakati, kwa usahihi na bila kuwepo udanganyifu wowote. Sambamba na hilo, Kamati inasisitiza umuhimu wa kuimarisha mifumo ya udhibiti wa vihatarishi kwa kufanya tathmini za mara kwa mara ili kuzuia hasara na kuhakikisha uendelevu wa Mfuko kwa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla, Kamati inaona kuwa makadirio ya mwaka 2026/2027 yanaonesha matarajio makubwa ya ukuaji wa mapato na kuimarika kwa taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango (WFM). Hata hivyo, mafanikio ya malengo haya yatategemea zaidi kuimarishwa kwa mifumo ya usimamizi wa mapato, matumizi sahihi ya teknolojia, uwajibikaji wa watendaji na usimamizi madhubuti wa rasilimali za umma. Kamati inaishauri Wizara na taasisi zake kuendelea kusimamia kwa karibu utekelezaji wa mipango hiyo ili kuhakikisha malengo yaliyowekwa yanafikiwa na mchango wa taasisi hizo katika maendeleo ya uchumi wa Zanzibar unaongezeka zaidi.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuhitimisha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa fursa hii adhimu ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu na kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango (WFM) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Kwa namna ya kipekee, nawapongeza na kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa wakati nikiwasilisha hotuba hii. Utulivu na usikivu wao ni kielelezo cha uwajibikaji na dhamira ya dhati ya kutekeleza wajibu wao kwa maslahi ya nchi yetu na wananchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Kamati yangu imefanya mapitio ya kina, kuchambua, kujadili na kuridhia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu yote saba (7) ya Wizara ya Fedha na Mipango (WFM) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, hivyo naomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waijadili bajeti hii na kutoa ushauri na mapendekezo yao na hatimaye waidhinishe makadirio hayo ili kuiwezesha Wizara ya Fedha na Mipango (WFM) kutekeleza kwa ufanisi majukumu na shughuli zake zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Kamati ya Bajeti, naunga

mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Ahsante sana,

…………………….

Mhe. Ali Suleiman Ameir,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar.**